# Vikundi vya Wakulima na Teknolojia

## Mafunzo kutoka Turiani, Morogoro and Mbozi, Mbeya



TARP II – SUA Project

**Waandishi**

Dk. J. G. Lyimo-Macha
Prof. E. K. Batamuzi

**Wahariri**

Kamati ya Mradi:

Prof. L. D. B. Kinabo
Prof. A. J. P. Tarimo
Prof. R. E. Malimbwi
Dk. P. J. Makungu

**ISBN9987 605 55 9**

**Kimechapishwa na:**

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa
Wakulima Wadogowadogo, Tanzania (TARP II – SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Chuo Kikuu, Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 4251

Toleo Namba: TS 2-33

**© 2002 TARP II – SUA Project**

Mbunifu wa Jalada - L.D.B. Kinabo: Picha inawaonyesha wakulima wakipata elimu kutoka kwa wenzao juu ya matumizi ya matrekta madogo katika utayarishaji ardhi.



# Yaliyomo

*Dibaji* *v*
*Vifupisho* *vii*

**1.0 Utangulizi** **1**

**2.0 Mifano Hai** **3**

**2.1. Kutembelea vikundi vya wakulima wa mpunga Mkindo Turiani** **3**

2.1.1. Vigezo vya kuchagua maeneo na wakulima 4
2.1.2. Waliyoyaona 5
2.1.3. Waliyojifunza 5
2.1.4. Hoja iliyojitokeza 7
2.1.5. Mambo ya kufuatilia yaliyopendekezwa na wakulima 8
2.1.6. Mapendekezo ya wawezeshaji 8

**2.2. Kutembelea vikundi vya wakulima na wafugaji wa wilaya ya Mbozi** 10

2.2.1. Vigezo vya kuchagua maeneo na wakulima 10
2.2.2. Waliyoyaona 12
2.2.3. Waliyojifunza 14
2.2.4. Hoja zilizojitokeza 15
2.2.5. Mambo ya kufuatilia yaliyopendekezwa na wakulima 15
2.2.6. Mapendekezo ya wawezeshaji 16

**3.0 Hitimisho** **18**

**4.0 Orodha ya washiriki** **19**

# Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula (MAFS), pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway (NLH), kinatekeleza Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogo wadogo Tanzania.

Lengo mojawapo katika mradi huu ni kuimarisha uhusiano kati ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Ugani. Ili kufikia lengo hili, mradi umepanga utaratibu wa kuwawezesha wakulima kutembeleana ndani ya kanda zao na kati ya kanda na kanda.

Makala hii inawasilisha ripoti ya ziara mbili zilizofanyika mwishoni mwa mwezi Oktoba na Novemba 2001. Ziara ya kwanza ya kimafunzo ya wakulima iliwashirikisha wakulima na washauri wa ugani kutoka wilaya za Kilosa, Kilombero, Rufiji na Morogoro Vijijini, ambao waliwatembelea wakulima wa mpunga wa Mkindo, Turiani wilaya ya Morogoro. Ziara ya pili iliwajumuisha wakulima na washauri wa ugani kutoka wilaya za Mbeya vijijini, Iringa Vijijini, Njombe, Ludewa na Chunya ambao walitembelea vikundi vya wakulima wa wilaya ya Mbozi. Taarifa hii pia inapatikana katika lugha ya kiingereza.

*Profesa L. D. B. Kinabo*
*Mratibu Mradi, TARP II-SUA*
*Novemba 2001*

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ARI | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo |
| EZ | Kanda ya Mashariki |
| MAFS | Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula |
| MBEPA | Chama cha Kuendeleza Nishati ya Gesi ya Samadi na Uhifadhi wa Mazingira Mbozi |
| NLH | Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway |
| SACCOS | Vyama vya Kuweka na Kukopa |
| SHZ | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini |
| SUA | Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo |
| TARP II | Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili |

# 1.0. UTANGULIZI

Uzoefu umeonyesha kuwa wakulima wadogowadogo huwa na uwezo na kufanya mambo makubwa na mara nyingi bila msaada kutoka nje ikiwa watajiunga pamoja katika vikundi vya uzalishaji. Hata misemo ya kawaida inaliweka hilo wazi, kwa mfano: "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu". Vilevile waswahili husema "Kidole kimoja hakivunji chawa".

Pamoja na faida za dhahiri zitokanazo na ushirikiano huo, jamii za kitanzania hazijatoa kipaumbele kwa mbinu hiyo kama njia ya kujikwamua kutokana na baa la njaa na umaskini. Kinyume chake jamii mbali mbali hutoa malalamiko mengi, kwa mfano, kuwa hawajaweza kufanya jambo fulani kutokana na kukosekana kwa mtaji au kuwa wamezalisha kwa wingi lakini hakuna soko. Utatuzi wa matatizo mengi, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mtaji na soko la uhakika, upo ndani ya uwezo wa wakulima. Sharti muhimu la kupata mafanikio ni kuunda vikundi.Vikundi vitawezesha kupata huduma mbali mbali kama elimu ya uzalishaji, kutafuta pembejeo na hata kutafuta soko kwa pamoja.

Kwa kutambua umuhimu wa uundaji na uendeshaji wa vikundi vya wakulima katika kuwakwamua kutokana na matatizo makuu, mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania, uliandaa na kutekeleza ziara ya mafunzo kwa wakulima toka sehemu mbali

mbali za kanda za Mashariki na Nyanda za Juu Kusini.

Ziara za mafunzo kwa wakulima zilifanyika katika kanda ya Mashariki kuanzia Novemba 11, 2001 hadi Novemba 14, 2001. Nyingine ilifanyika kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuanzia Oktoba 29, 2001 hadi Novemba 1, 2001. Katika kanda ya Mashariki, wakulima na wataalamu wa ugani kutoka wilaya za Kilombero, Kilosa, Rufiji na Morogoro waliwatembelea wenzao wa Mkindo, Turiani ili kubadilishana uzoefu na elimu kuhusu kilimo cha umwagiliaji cha mpunga na umuhimu wa kuwa na vikundi vya wakulima katika kutekeleza shughuli hizo. Huko kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wakulima na wataalamu wa ugani kutoka wilaya za Njombe, Mbeya, Iringa, Ludewa na Chunya walibadilishana elimu na uzoefu wao na wakulima wa wilaya ya Mbozi katika shughuli za: uendeshaji wa vyama /vikundi vya wakulima na wafugaji, vyama vya kuweka na kukopa, uzalishaji wa kahawa bora, matumizi ya nishati ya gesi ya samadi na utafutaji wa soko la maziwa.

Katika makala hii, maelezo yametolewa kuhusu mambo ambayo washiriki wa ziara waliyaona, waliyojifunza na mapendekezo yao ya shughuli ambazo wameahidi kuzifanya kutokana na mafunzo waliyoyapata katika ziara hizi. Yote haya yakiwa na lengo la kuimarisha uelewa wetu wa faida za uimarishwaji wa uhusiano kati ya wakulima, watafiti



na wataalamu wa ugani kwa kupitia ziara za mafunzo kwa wakulima.

## 2.0. MIFANO HAI

### 2.1. Kutembelea vikundi vya wakulima wa mpunga katika eneo la Mkindo Turiani

Wakulima ishirini na wawili (wanawake 10 na wanaume 12) na mabwana shamba wawili kutoka wilaya za Kilombero, Rufiji, Kilosa na Morogoro waliwatembelea wakulima wa mpunga wa eneo la Mkindo lililopo Turiani kuanzia Novemba 11, 2001 hadi Novemba 14, 2001. Malengo ya ziara hii yalitokana na warsha ya pili ya wakulima wa Kanda ya Mashariki iliyofanyika VETA-Mikumi mwezi Aprili 2001. Lengo kuu lilikuwa kuwawezesha wakulima kupata elimu na mawazo juu ya kilimo asili cha umwagiliaji cha mpunga, kwa kupitia mfumo wa kupashana na kubadilishana habari na wakulima wenzao wa eneo la Mkindo. Vile vile wakulima hao walipata nafasi ya mafunzo mafupi yaliyotolewa na mkuu wa kituo cha mafunzo ya Wakulima cha Mkindo. Mwishoni mwa ziara wakulima walifaidika kwa kutunukiwa vyeti vya kuhudhuria mafunzo hayo.

### 2.1.1 Vigezo vya kuchagua maeneo na wakulima

*Uchaguzi wa eneo*

Uchaguzi wa eneo ulizingatia, kwanza, mada muhimu na malengo yaliyojitokeza wakati wa warsha ya pili ya kanda ya mashariki. Pili, kuwepo kwa kituo cha mafunzo ya wakulima cha Mkindo ambacho kinatoa mafunzo juu ya kilimo cha umwagiliaji cha mpunga.

*Uchaguzi wa Wakulima*

Wakulima ishirini na wawili walichaguliwa kwa kutumia vigezo vya kuchagua nani aende vilivyopo kwenye chapisho lenya namba TS2-28 la Oktoba 2001 lililotayarishwa na mradi wa TARP II-SUA. Chapisho hilo limeelezea na kutilia mkazo vigezo vifuatavyo: ubunifu, uhusiano na vikundi au vyama vya wakulima (Wanachama wa vikundi vya uzalishaji ambao vikundi vyao vipo katika hatua za awali na pia ambavyo bado havijawa na maendeleo bayana, kutokana na kutokuwa na katiba za vikundi, havijaandikishwa na havina miradi thabiti), awe na uwezo wa kuelewa na kueleza wengine kile alichojifunza ili kutimiza lengo la ziara hii na pia jinsia.

Kikundi hiki cha wakulima kilishirikisha wataalamu wa ugani wawili, moja kutoka Rufiji na mwingine Ifakara. Pia kikundi kiliambatana na watafiti wawili



kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na mmoja kutoka ARI-Ilonga.

### 2.1.2 Waliyoyaona

*Mambo ya msingi*

- Utayarishaji wa ardhi kwa kutumia jembe la mkono (kukatua) na pia kwa kutumia matrekta madogo (power tillers)
- Vitalu vya mpunga
- Mbinu mbalimbali za kuhifadhi vyanzo vya maji
- Utayarishaji wa vitalu vya micha ya mpunga

*Mengineyo*

- Mbinu zilizoboreshwa za kutunza, kuandaa/kutayarisha na kuhifadhi mbegu.
- Utunzaji wa rutuba katika udongo na matumizi ya mbolea kwenye mashamba ya mpunga.
- Matumizi ya vikundi vya wakulima kama njia ya kitaalam ya kusambaza teknolojia.
- Utunzaji wa mifereji ya umwagiliaji ya asili na ile iliyoboreshwa.

### 2.1.3 Waliyojifunza

Katika ziara hii wakulima walijifunza mambo yafuatayo

- Aina mbalimbali za mpunga

- Umuhimu wa kuunda na kufanya kazi kwa vikundi vya wakulima
- Utunzaji wa maji katika mashamba ya mpunga
- Umuhimu wa uchaguzi na uandaaji wa mbegu
- Ujuzi wa kuandaa kitalu
- Jinsi ya kutumia mashine (power tillers) na jembe la mkono katika kukatua, kuchanganya na kusawazisha udongo.
- Umuhimu wa kupandikiza miche ya mpunga
- Njia mbalimbali zinazotumika kuvuna mpunga
- Hatua za kukusanya na kuweka kumbukumbu za takwimu mbali mbali katika mashamba ya mpunga (AESA).
- Mbinu za kuzuia wadudu na magonjwa ya mpunga
- Utunzaji wa rutuba ya ardhi na matumizi ya mbolea.
- Magugu ya mpunga (kwa mfano, Pungapunga).



50031648072



*Picha hii inawaonesha wakulima wakiangalia mifereji ya umwagiliaji katika mashamba ya mpunga*

### 2.1.4 Hoja iliyojitokeza

Hoja ifuatavyo ilijitokeza kwenye ziara hii ya wakulima

- Muda uliopangwa kwa shughuli za mazoezi mashambani ulikuwa mfupi sana kuweza kufaidika zaidi na mafunzo.

## 2.1.5 Mambo ya kufuatilia yaliyopendekezwa na wakulima Wakulima waliahidi kutimiza mambo yafuatayo mara watakaporudi majumbani kwao

- Kuchagua, kuandaa mbegu na vitalu kwa kufuata maelekezo waliyojifunza
- Kutunza mashamba yao ya mpunga kwa kutumia njia bora kama wanazotumia wakulima wa eneo la Mkindo, Turiani
- Kufanya kazi katika vikundi (Vikundi vya wakulima) ili kutumia muda wao vizuri na kurahisisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo (mfano power tillers).
- Kutengeneza mifereji mizuri ya umwagiliaji na kutunza maji vizuri katika majaluba ya mpunga kama walivyofundishwa.
- Kuunda vikundi vya wakulima kwa ajili ya kutumia maji vizuri kutoka kwenye vyanzo.

## 2.1.6 Mapendekezo ya wawezeshaji wa ziara

- Katika safari za ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za mradi iwepo pia shughuli ya kufuatilia ahadi zilizotolewa na wakulima ili kuona maendeleo ya upokeaji wa teknolojia walizojifunza katika ziara. Ona kipengele hapo juu (2.1.5)





*Picha hii inawaonesha wakulima wakiangalia vitalu vya mpunga na aina za mpunga*

## 2.2. Kutembelea vikundi vya wakulima na wafugaji wa wilaya ya Mbozi

Wakulima tisa (wanawake 5 na wanaume 4) kutoka wilaya za Mbeya vijijini, Iringa vijijini, Njombe, Chunya na Ludewa wakifuatana na wataalamu wa ugani, waliwatembelea wakulima walio katika vikundi vya uzalishaji vya wilaya ya Mbozi kuanzia Oktoba 29 hadi Novemba 1, 2001. Ziara hii ililenga kutoa nafasi kwa wakulima kuona jinsi vikundi vya uzalishaji vinavyoundwa, kundeshwa, faida na mapungufu yake. Ikumbukwe kuwa wilaya ya Mbozi na hasa Mbozi Mashariki imepiga hatua kubwa katika uundaji wa vikundi vizuri vya wakulima.

### 2.2.1 Vigezo vya kuchagua maeneo na wakulima

*Uchaguzi wa eneo*

Eneo lilichaguliwa kutokana na umuhimu wake kwa kukidhi mahitaji ya mada iliyopendekezwa wakati wa warsha za wakulima zilizofanyika Njombe Novemba 2000, na Sumbawanga June 2001. Wakati wa warsha hizo, uundaji na uendeshaji wa vikundi vya wakulima ulipendekezwa kama utatuzi wa matatizo kama vile ukosefu wa soko la mazao ya kilimo/mifugo na ukosefu wa huduma za mikopo kwa wakulima wadogo wadogo.Vile vile, eneo lililochaguliwa lina vikundi vingi,vyama vya uzalishaji (kwa mfano; Benki kata, vikundi vya ufugaji na uuzaji maziwa na



vikundi vya uboreshaji wa mazao ya biashara na soko), na pia wakulima wa maeneo hayo wanao uzoefu mkubwa kuhusu maswala hayo.

Pia eneo lililotembelewa lina wakulima wenye uzoefu wa matumizi ya nishati mbadala kwa mfano, gesi ya samadi, jiko aina ya "upesi"na uchomaji wa matofali kwa kutumia pumba za mpunga.

*Uchaguzi wa Wakulima*

Wakulima tisa walichaguliwa kwa kutumia vigezo vya kuchagua nani aende vilivyopo kwenye chapisho lenye namba TS2-28 la Oktoba 2001 lililotayarishwa na mradi wa TARP II-SUA. Chapisho hilo limeelezea na kutilia mkazo vigezo vifuatavyo: ubunifu, uhusiano na vikundi au vyama vya wakulima (Wanachama wa vikundi vya uzalishaji ambao vikundi vyao vipo katika hatua za awali na pia ambavyo bado havijawa na maendeleo bayana, kutokana na kutokuwa na katiba za vikundi, havijaandikishwa na havina miradi thabiti), awe na uwezo wa kuelewa na kueleza wengine kile alichojifunza ili kutimiza lengo la ziara hii na pia jinsia.
Msafara ulijumuisha pia wataalamu wa ugani wanne kutoka Mbozi, watafiti watatu kutoka SUA, na watafiti wawili kutoka kituo cha utafiti wa kilimo Uyole.

### 2.2.2. Waliyoyaona


*Mambo ya msingi*

- Wakulima walijifunza namna za kuunda na kuendeleza vikundi mbali mbali vya uzalishaji.
- Utunzaji wa mazingira.
- Uundaji na uendeshaji wa Benki Kata (SACCOS).
- Muundo wa vikundi vya uboreshaji wa mazao ya biashara (kwa mfano kahawa)
- Walijifunza mbinu za kurahisisha upatikanaji wa pembejeo na soko.
- Uundaji wa vikundi vya wafungaji wa ngómbe wa maziwa, kuboresha mbinu za kuongeza muda wa kuhifadhi maziwa na kupata soko la pamoja na la uhakika.
- Jinsi ya kutumia vikundi vya wakulima kurahisisha upatikanaji wa elimu na teknolojia kama vile jinsi ya kutengeneza mtambo wa nishati ya gesi ya samadi.
- Utengenezaji na matumizi ya majiko ya upesi (Majiko yanayotumia kuni chache).
- Uundaji na uendeshaji wa vikundi vya kina mama vya ufugaji wa mbuzi wa maziwa



*Mengineyo*

- Matumizi ya pumba za mpunga kwa ajili ya kuchomea tofali
- Uchanganyaji wa chakula cha nguruwe kutumia vyakula vyenye viini lishe vilivyopendekezwa kitaalamu ili kuongeza ubora wa wanyama na kupunguza gharama za uzalishaji.
- Kilimo hai.



*Matumizi ya nishati mbadala kama ya gesi ya samadi ni mojawapo ya njia muhimu za kupunguza adha kwa akina mama na uharibifu wa mazingira.*

### 2.2.3 Waliyojifunza

Kutokana na ziara hii wakulima walikiri kujifunza mambo mengi yahusuyo vikundi vya wakulima na pia mbinu bora za kilimo, ufugaji na matumizi ya nishati mbadala. Yafuatayo ni baadhi ya mambo waliyojifunza

- Kuunda vikundi kunawawezesha wakulima na wafugaji kutatua tatizo la ukosefu wa mtaji wakati wa kuanzisha na kuendeleza miradi ya binafsi na jumla.
- Uundaji wa vikundi unatatua tatizo sugu la ukosefu wa soko la uhakika kwa mazao ya kilimo na mifugo.
- Kuwa na huduma za kifedha karibu na wakulima, kwa mfano vyama vya akiba na mikopo ni ukombozi wa wakulima na wafugaji wadogo wadogo.
- Umoja wa wakulima na wafugaji ukizingatiwa utaondoa umasikini katika kaya na utaongeza pato la kaya.
- Mkulima mdogo anao uwezo wa kutumia nishati mbadala kama ya gesi ya samadi na kwa njia hiyo atapunguza adha kwa akina mama na uharibifu wa mazingira.
- Ufugaji wa mbuzi wa maziwa unawezekana hata kwenye eneo lenye maeneo madogo ya malisho.
- Ujenzi wa mtambo wa nishati ya gesi ya samadi.
- Umuhimu wa kutunza kumbu kumbu na taarifa zote za vikundi vya wakulima



### 2.2.4. Hoja zilizojitokeza

Kutokana na waliyoyaona, wakulima walitoa hoja zifuatazo

- Ili kuleta unafuu kwa wakulima ni vyema nauli zitumwe wilayani kwao mapema na wazipate kabla ya safari. Utaratibu wa sasa ambapo mkulima hujitegemea nauli na halafu kurudishiwa baadaye siyo mzuri.
- Muda uliopangwa kwa ajili ya ziara ni mdogo mno hasa ikizingatiwa kuwa mambo ya kujifunza ni mengi.
- Wapatiwe elimu zaidi kuhusu nishati mbadala (biogas)

### 2.2.5. Mambo ya kufuatilia yaliyopendekezwa na wakulima

Wakulima walitoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha ziara zijazo

- Muda wa ziara za mafunzo uongezwe kwani mambo ya kujifunza ni mengi.
- Ikiwezekana ziara zifanyike wakati wa msimu wa kilimo ili wakulima wageni washiriki kwa vitendo katika kazi za uzalishaji
- Kamati ya utekelezaji/usimamizi wa mradi unakaribishwa kata ya Mdabulo, wilaya ya Mufindi ili kuona shughuli za vikundi na kuwatembelea waliofaidika na ziara hii.

- ❖ Vituo vya utafiti vilivyopo katika maeneo husika vipangiwe ratiba /utaratibu wa kuvitembelea ili kupata elimu zaidi
- ❖ Wazalishaji wa Mbozi wahamasishwe katika shughuli za kilimo hai na matumizi ya madawa asili.

Wakulima pia waliahidi kufanya yafuatayo mara warudipo vijijini kwao:


- ❖ Kuanzisha na kuendeleza ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa
- ❖ Kutengeneza mitambo ya gesi
- ❖ Kuhamasisha wenzao na kuanzisha benki kata
- ❖ Kutengeneza na kutumia majiko ya "upesi".

### 2.2.6. Mapendekezo ya wawezeshaji wa ziara

- ❖ Muda wa ziara uwe wiki moja ili kutoa nafasi ya kutosha kwa wageni na wenyeji kujifunza vya kutosha.
- ❖ Vituo vya utafiti/mafunzo ya kilimo mifugo na ushirika katika eneo lililotembelewa vihusishwe katika kutembelewa wakati wa ziara. Ingefaa vituo hivi vitembelewe mwishoni mwa ziara ili wageni na wenyeji wajifunze mbinu bora na za kitaalamu.
- ❖ Ziara hizi zifanyike wakati wa msimu ili washiriki waweze kuona vitu/mambo mengi hasa shughuli za vikundi.



- ❖ Ziara ziendelezwe ili kuweka chachu kwa ajili ya miradi endelevu katika jamii kwani kila mtu anatamani kufanya jambo lenye kumnufaisha.
- ❖ Vipeperushi viandaliwe kwa kutoa elimu zaidi kuhusu mada zinazoendana na madhumuni ya miradi iliyopo kwa mfano, nishati ya gesi ya samadi (Biogas).



*Ufugaji bora wa ngombe wa maziwa ni muhimu katika kutunza afya ya jamii na kuongeza kipato cha kaya*

## 3.0. Hitimisho

Ziara hizi mbili zimeleta mwanga na changamoto kwa watafiti, wataalamu wa ugani na wakulima kuhusu umuhimu na faida zinazopatikana kwa kuwa na vikundi vya uzalishaji vya wakulima na wafugaji. Kwa ujumla imeonekana kuwa vikundi hivi vimewawezesha wakulima kupata maendeleo (wengine dalili za maendeleo) kwa urahisi hasa katika nyanja za upatikanaji wa pembejeo na masoko ya mazao yao. Huduma muhimu kama vile elimu na ushauri pia zilipatikana kwa wakati muafaka kwa sababu ya ushirikiano mzuri uliokuwepo kati ya vikundi vya wakulima na wataalamu wa ugani wa maeneo hayo. Washiriki pamoja na wawezeshaji wamekubaliana kimsingi kuwa vikundi vya wakulima na wafugaji ni muhimu katika kuleta uhakika wa chakula na ongezekeo la pato la kaya



## 4.0. Orodha ya washiriki

### 4.1. Turiani

| Na. | Jina <u>Wakulima</u> | Jinsia | Kijiji | Anuani |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Hamisi J. Funge | Me | Mkindo | S.L.P 96, Turiani, Morogoro |
| 2. | Tabu John | Ke | Wami-Dakawa | S.L.P 612, Morogoro |
| 3. | Frederick Ndikwege | Me | Njagi | S.L.P 214, Ifakara, Morogoro |
| 4. | Rajabu Makunja | Me | Wami-Dakawa | S.L.P 612, Morogoro |
| 5. | Hamida Gonga | Ke | Mvumi | S.L.P 173, Kilosa, Morogoro |
| 6. | Sikuzani Ramadhani | Ke | Mkindo | S.L.P 96, Turiani, Morogoro |
| 7. | John Mgimba | Me | Njagi | S.L.P 214, Ifakara, Morogoro |
| 8. | Hilda Raphael | Ke | Dihombo | S.L.P 130, Turiani, Morogoro |
| 9. | Edward Masolwa | Me | Mkula | S.L.P 8, Mang'ula, Morogoro |
| 10. | Boniface Joseph | Me | Dihombo | S.L.P 130, Turiani, Morogoro |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | Ally Mtunga | Me | Mkula | S.L.P 8, Mang'ula, Morogoro |
| 12. | Hamza Haji | Me | Mvumi | S.L.P 173, Kilosa, Morogoro |
| 13. | Athumani S. Hamadi | Me | Ikwiriri | S.L.P 36, Rufiji, Pwani |
| 14. | Mariamu S. Mketo | Ke | Bunju-Ikwiriri | S.L.P 14, Rufiji, Pwani |
| 15. | Mwajabu Athumani | Ke | Ikwiriri | S.L.P 64, Rufiji, Pwani |
| 16. | Theresia Kipanga | Ke | Msalabani | S.L.P 98, Ilonga, Kilosa |
| 17. | Athumani Kijazi | Me | Njagi | S.L.P 214, Ifakara, Morogoro |
| 18. | Asha Mate | Ke | Mvumi | S.L.P 173, Kilosa, Morogoro |
| 19. | Hashim S. Muhenga | Me | Ikwiriri | S.L.P 14, Rufiji, Pwani |
| 20. | Rose Matulu | Ke | Msalabani | S.L.P 98, Ilonga, Kilosa |
| 21. | Mwajuma Milando | Ke | Mkula | S.L.P 8, Mang'ula, Morogoro |
| 22. | Justin Mkumbae | Me | Msalabani | S.L.P 98, Ilonga, |



Kilosa

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Wataalamu wa ugani** | | | |
| 1. | Aziz Msangi | Me | Ikwiriri | S.L.P 64, Rufiji, Pwani |
| 2. | Hashim Semkuya | Me | Mkula | S.L.P 8, Mang'ula, Morogoro |

### 4.2. Mbozi

| Na. | Jina | Jinsia | Kijiji | Anuani |
|---|---|---|---|---|
| | **Wakulima** | | | |
| 1. | George Mwansenga | Me | Kibaoni | S.L.P 8, Chunya, Mbeya |
| 2. | Innocent Mbawala | Me | Ludewa | S.L.P 50, Ludewa, Mbeya |
| 3. | Agnes Mwihava | Ke | Kibaoni | S.L.P 8, Chunya, Mbeya |
| 4. | Charles Jimiston | Me | Bwawani | S.L.P 179, Umalila, Mbeya |
| 5. | Cordula D. Mtweve | Ke | Itundu | S.L.P Itundu, Malangali, Iringa |
| 6. | Ester Nyinge | Ke | Kihorogota | S.L.P 108, Isimani, Iringa |



LIBRARY DATE 23/4/2002

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7. | Lawrence M. Mgova | Me | Kilolo | S.L.P 890, Kilolo, Iringa |
| 8. | Bahati W. Mhapa | Ke | Ihefu | S.L.P 142, Mafinga, Iringa |
| 9. | Theresia Yohana | Ke | Mbawi | S.L.P 179, Ilembo, Mbeya |
| | **<u>Wataalamu wa ugani</u>** | | | |
| 1. | Peter Lanjau | Me | DALDOs off. | S.L.P 94, Mbozi, Mbeya |
| 2. | Deo Rwechungura | Me | DALDOs off. | S.L.P 190, Mbozi, Mbeya |
| 3. | Emma Moshi | Ke | MBEPA | S.L.P 209, Mbozi, Mbeya |
| 4. | R. Kimbi (Kimboi) | Ke | DALDOs off. | S.L.P 94, Mbozi, Mbeya |

**Ufunguo:**

Ke - Mwanamke
Me - Mwanaume



LIBRARY DATE 23/4/2002 ... ARTS COLLEGE